

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
O.R. TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO  
0626810261/ 0652178559 MKUU WA SHULE  
0782431574 MAKAMU**

SHULE YA SEKONDARI GARE  
S.L.P 134  
LUSHOTO  
TAR\_\_\_\_\_

MZAZI WA \_\_\_\_\_  
S.L.P. \_\_\_\_\_  
LUSHOTO

**YAH. MAELEKEZO YAA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GARE KWA MWAKA  
2021**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika Shule hii **mwaka 2021**. Shule ya Sekondari GARE ipo umbali wa KILOMITA KUMI NA SABA (17km) kutoka makao makuu ya halmashauri ya Lushoto

Muhula wa masomo unaanza tarehe 11.01.2021 hivyo mwanao atatakiwa kuripoti shuleni siku ya kufungua shule mwisho wa kuripoti ndani ya wiki moja toka tarehe ya kufungua shule.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**A. SARE ZA SHULE (WAVULANA)**

- (i) Suruali nyeusi mbili, kitambaa kizito (upana wa suruali size 16), shati nyeupe mikono mifupi mbili, viatu nyeusi vya ngozi vinavyofungwa kamba jozi mbili, sweta mbili za rangi ya kijivu na soksi nyeusi za kutosha.
- (ii) Rain boot nyeusi kwa ajili ya wakati wa mvua.

**WASICHANA**

- (i) sketi nyeusi mbili ziwe ndefu(mshono wa rinda box) mashati meupe mawili mikono mifupi. Kwa wanafunzi wa kiislam sketi iwe ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu. Hijabu nyeupe isiwe kitambaa cha mpira jozi mbili zenye stara. Sweta la kijivu jozi mbili.(suruali kwa wasichana hazitaruhusiwa)
- (ii) soksi nyeupe za kutosha
- (iii) rain boot nyeusi wakati wa mvua

**B: SARE ZA MICHEZO**

Sare za michezo kwa wote ni tract suit blue yenye mistari myeupe jozi moja.

**C. VIFAA VYA TAALUMA**

- (i) Daftari kubwa 10 (quire 3)
- (ii) daftari ndogo 10 kwa ajili ya mitihani ya wiki
- (iii) Kalamu na penseli za kutosha
- (iv) rula na mkebe
- (v) kamusi ndogo ya English to English
- (vi) Begi la kubebea daftari ambalo ni imara

#### **D. VIFAA VYA SHAMBA NA USAFI SHULENI**

Mwanafunzi awe na jembe jipya lenye mpini na ndoo ndogo moja mpya.

#### **E: CHAKULA**

Shule ya sekondari Gare inatoa chakula cha mchana ambacho ni makubaliano ya wazazi. Ambapo kila mzazi analeta kilo 10 za mahindi yaliyokobolewa, maharage kilo 04. Hivyo utakapomleta hakikisha unatimiza wajibu wako kwa kuwaunga mkono wazazi wenzako kuleta chakula ili kuhakikisha mtoto anakula shuleni.

#### **Hivyo mtoto awe na sahani/bakuli na kijiko kwa ajili ya chakula**

NB: fomu ya Daktari na sheria za shule zimeambatanishwa. Fomu ya maelezo binafsi itatolewa siku ya kufungua shule.

Ndugu mzazi hakikisha unafanya maandalizi ya kutosha na kwa wakati kwa ajili ya kumuandaa mwanao kitaaluma.

Nikutakie maandalizi mema

---

**KASIANI B. MASHAMBO**  
**MKUU WA SHULE**

**STUDENT MEDICAL CERTIFICATE**

To be completed by the Government Medical Officer and return to the Headmaster of  
Gare Secondary School BOX 134. Lushoto

Date.....

**To the medical officer**

.....  
.....  
.....

Re.....

Please examine the student mentioned above and comment on his health by responding to  
the following items. Kindly put a tick or cross in front of either Yes or No

1. Does the student have the problem in connection with

a) Sight?.....No ( ) Yes ( )

If Yes state and  
recommend.....

b) Hearing?..... No ( ) Yes ( )

If Yes state and recommend.....

c) Speech?..... No ( ) Yes ( )

If Yes state and  
recommend.....

TB? ..... No ( ) Yes ( )

If Yes state and  
recommend.....

.....

BP?..... No ( ) Yes ( )

If Yes state and  
recommend.....

Any other disability?..... No ( ) Yes ( )

if Yes state and  
recommend.....

.....

What is your recommendation on the said student medical fit for studying at this school

.....  
.....  
.....

MEDICAL OFFICER'S NAME \_\_\_\_\_

SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP \_\_\_\_\_

## **MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE**

- i. Wizi
- ii. Utoro( kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
- iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo
- iv. Kutoa lugha chafu kwa walimu/walezi au kwa mmwanafunzi mwenzake na jamii kwa ujumla
- v. Kupiga au kupigana
- vi. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
- vii. Uvutaji wa sigara
- viii. Uaesharati,uhusiano wa jinsia moja kuoa au kuolewa
- ix. Kushiriki matendo ya kihalifu, siasa na matendo mengine yoyote yanayovunja sheria ya nchi
- x. Kupata au kusababisha mimba
- xi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba zakulala wageni
- xii. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi ndani na nje ya MAZINGIRA YA SHULE
- xiii. Kudharau bendera ya Taifa
- xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiuwa au kutishia kujiuwa kama kunywa sumu na mengineyo
- xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
- xvi. Kutohudhuria vipindi vya dini ambavyo vipo kwa mujibu wa sheria na kanuni za shule.
- xvii. Kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa